

?Home > Kutoa Au Kuomba Sadaka > 23. Maskini Au Mwombaji Asaidiwe Mara Ngapi

.Baada ya kumsaidia masikini mara tatu unaweza kumwambia aondoke

Walid bin Sabih anasema kuwa: .1

“Siku moja mimi nilikuwa kwa Al Imam Ja’afir as-Sadiq a.s. na hapo akatokezea mwombaji mmoja. Imam a.s alimpa chochote huyo mwombaji na akatokezea mwombaji wa pili naye akapewa chochote. Hivyo hivyo akatokezea mwombaji wa nne basi Al Imam a.s akamwambia Allah atakusaidia upate zaidi njia yako atakupanulia. Na baada ya hapo Imam a.s akasema iwapo mtu atakuwa na Dirham takriban elfu thelathini au arobaini, na akanuia akawa na mpango wa kuzitumia zote ambazo kimatokeo hatabakiwa na chochote basi mtu kama huyo atawekwa mionganii mwa wale watu ambaa Allah swt ”.huzitupilia mbali dua zao

Kwa hayo mimi nikasema,

?“Ewe mwana wa Mtume wa Allah.! Je! ni makundi gani ya watu hawa watatu

Kwa hayo Imam a.s akajibu,

“Mmoja wao ni yule ambaye ana mapesa na mali na baada ya kutumia vyote anaomba ‘ewe Mola wangu naomba unipe riziki’. Basi hapo Allah swt anamjibu ‘Je! mimi sikukupanulia njia na kukuwekea ”?sababu za wewe kujekeea riziki yako

Ali ibn Hamza anasema kuwa: .2

”Katika kujibu swalii (aliyoulizwa), mimi nilimsikia Al Imam Ja’afir as-Sadiq a.s akisema mwalishe watatu - na kama mnataka kuwapa chochote zaidi muwape ama sivyo nyie mmeshatimiza haki ya siku yenu . ”hiyo

Source URL:

<https://www.al-islam.org/ar/kutoa-au-kuomba-sadaka-shaykh-hurr-al-aamili/23-maskini-au-mwombaji-asaidiwe-mara-ngapi>